



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**



(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji(W))

**Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na.KDC/F.20/46/48**

15 Novemba, 2024

**YAH: TANGAZO LA MAOMBI YA MKOPO UNAOTOLEWA NA WIZARA
YA FEDHA**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji imepokea mgao wa Fedha kiasi cha Tsh. **403,273,817.84** (milioni mianne na tatu mia mbili sabini na tatu elfu mia nane kumi na saba na senti themanini na nne) kutoka Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununua Magari/Pikipiki, samani na matengenezo ya magari na pikipiki kwa Watumishi. Mikopo hiyo inatolewa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na mkopo huo hauna riba. Masharti na Vigezo vya Mkopo huo ni kama ifuatavyo;

1. Mkopaji (Mtumishi) anatakiwa awe amethibitishwa kazini
2. Mkopaji (Mtumishi) anatakiwa kubakiwa na theluthi moja (1/3) ya Mshahara wake baada ya makato yote.
3. Mkopaji (Mtumishi) hataruhusiwa kukopeshwa mkopo mwingine hadi atakapomaliza kulipa deni la awali.
4. Mkopaji (Mtumishi) atatakiwa kujisajili HAZINA PORTAL kwa kutumia link **als.muse.go.tz** ndiyo itakayomuwezesha kutuma maombi ya Mkopo kwa Mwajiri (Mkurugenzi Mtendaji).
5. Mkopaji (Mtumishi) atarejesha mkopo aliokopa kwa kipindi cha muda usiozidi Miezi sabini na Mbili (72) ambayo ni sawa na miaka sita

6. Mkopaji (Mtumishi) atakopeshwa kulingana na kiwango chake cha Mshahara.

7. Mkopaji (Mtumishi) atalipia 'service charge' ambayo ni 3% na anatakiwa kuchangia bima (Protection Fund) ambayo ni 1%.

Watumishi wote wenye sifa mnakaribishwa kujisajili na kutuma maombi kupitia als.muse.go.tz kwa muda kuanzia tarehe 15/11/2024 hadi tarehe 21/11/2024.

Tangazo hili limetolewa na;



Beatrice R. Dominic

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMSAHAURI YA WILAYA YA KISARAWA

